**OFISI YA RAIS**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA**

**Kumb.Na. GDC/I.20/9/65** **06-09-2025**

# TANGAZO LA KUITWA KWENYE USAILI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Geita anapenda kuwataarifu Waombaji Kazi wote walioomba kazi kuwa usaili unatarajiwa kuendeshwa kuanzia tarehe **09/09/2025 hadi tarehe 10/09/2025** na hatimaye kuwapangia vituo vya kazi waombaji kazi watakaofaulu usaili huo.Wasailiwa wanaoitwa kwenye usaili wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:-

1. Usaili utafanyika kuanzia tarehe kama ilivyooneshwa kwenye tangazo hili muda na sehemu ambapo usaili utafanyika umeainishwa kwa kila Kada.
2. Kila msailiwa anatakiwa kufika kwenye eneo la usaili akiwa amevaa mavazi nadhifu
3. Kila Msailiwa anapaswa kuwa na kitambulisho kwa ajili ya utambuzi;
4. Vitambulisho vinavyokubalika ni pamoja na:- Kitambulisho cha Taifa (NIDA) Kitambulisho cha Mkazi, Kitambulisho cha Mpiga kura,Kitambulisho cha kazi, Leseni ya Udereva,Hati ya kusafiria na Barua ya Utambulisho toka Serikali ya Kijiji/Mtaa.
5. Wasailiwa wanatakiwa kufika na **VYETI VYAO HALISI, kuanzia cheti cha kuzaliwa,kidato cha IV, VI, Stashahada,Stashahada ya Juu, Shahada na kuendelea kutegemeana na sifa za Mwombaji**.
6. Wasailiwa watakaowasilisha **Testimonials, Provisional Results, Statement of results, hati za matokeo za kidato cha IV na VI (form V and form VI results slips) HAVITAKUBALIWA NA HAWATARUHUSIWA KUENDELEA NA USAILI**.
7. Kila msailiwa atajigharamia kwa Chakula, Usafiri na Malazi.
8. Kila Msailiwa azingatie tarehe, muda na mahali alipopangiwa kufanyia usaili.
9. Kwa waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe Vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (kama TCU, NACTE au NECTA)
10. Waombaji kazi ambao majina yao hayakuonekana katika tangazo hili watambue kuwa hawakukidhi vigezo. Hivyo, wasisite kuomba tena pindi nafasi za kazi zitakapotangazwa na kuzingatia mahitaji ya tangazo husika.
11. **Kwa kada ambazo wanatakiwa kusajiliwa na Bodi zao za Kitaaluma wanapaswa kuja na vyeti vyao Halisi vya Usajili pamoja na Leseni za kufanyia kazi.**
12. Wasailiwa wote walioitwa kwenye usaili wahakikishe wanaingia kwenye akaunti zao na kunakili namba ya mtihani kwa kuwa namba hizo hazitatolewa siku ya usaili
13. Wasailiwa wote mnajulishwa kuwa hali ya hewa ya Wilaya ya Geita ni jua wakati wa mchana na baridi wakati wa jioni, usiku na asubuhi hivyo mnashauriwa kuwa na nguo zinazostahimili mazingira hayo.

## RATIBA YA USAILI WA VITENDO

| MWAJIRI | KADA | TAREHE YA USAILI | MAHALI |
|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Geita | DEREVA DARAJA II | 09-09-2025 07:00 AM | HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA - NZERA |

## RATIBA YA USAILI WA MAHOJIANO

| MWAJIRI | KADA | TAREHE YA USAILI | MAHALI |
|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Wilaya ya Geita | DEREVA DARAJA II | 10-09-2025 07:00 AM | UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA - NZERA |

**MWAJIRI:** HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA
**KADA:** DEREVA DARAJA II
**TAREHE YA USAILI WA MCHUJO:** HAKUNA
**MAHALI:** HAKUNA
**TAREHE YA USAILI WA VITENDO:** 09-09-2025 07:00 AM
**MAHALI:** HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA - NZERA
**TAREHE YA USAILI WA MAHOJIANO:** 10-09-2025 07:00 AM
**MAHALI:** UKUMBI WA HALMASHAURI YA WILAYA YA GEITA - NZERA

| # | JINA LA MWOMBAJI | ANUANI |
|---|---|---|
| 1 | BARAKA LUCAS MSENGI | P.O Box 615, Korogwe, Tanga |

**LIMETOLEWA NA;**

**MKURUGENZI MTENDAJI**